**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari Muyovozi**

**S.L.P 463**

**Kasulu**

**Tarehe ……………….**

**Namba za Simu………………….**

**Mkuu wa Shule:0757932910/0622032538**

**Makamu Mkuu wa Shule:0612713058**

**Matron/Patron:0744464130**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUYOVOZI HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU MKOA WA KIGOMA MWAKA ………………….**

## 1. Utangulizi

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka …………………… tahasusi ya …………..

Shule ipo Kilometa 44 Kutoka Kasulu Mjini kuelekea barabara kuu iendayo Kibondo, Mwanza, Arusha, Moshi, Singida, Dar Es Salaam n.k. Mwanafunzi ili afike shuleni anatakiwa ashuke kituo cha **Mgombe** sokoni kama anatokea Kasulu Mjini au ashukie kituo cha njia panda ya kwenda Kambi ya jeshi la kujenga Taifa **(JKT) Mtabila** katika kijiji cha Mgombe. Ambapo nauli kutoka Kasulu Mjini hadi Mgombe sokoni ni shilingi elfu tatu (3,000/=) kwa magari madogo ya abiria na shilingi elfu Saba (7,000/=) kwa pikipiki kutoka Mgombe

hadi shuleni. Pia unaweza kukodi usafiri au gari dogo kutokea Kasulu Mjini kwa shilingi elfu arobaini (40,000/=) inategemea na makubaliano yenu.

Kwa wanafunzi wanaotokea mikoa mbalimbali na kupita njia ya Kahama Kibondo,hakuna sababu ya kufika Kasulu mjini bali shuka moja kwa moja kwnye **kibao cha JKT Mtabila na panda pikipiki(Bodaboda**) njoo shuleni na zinapatikana mda wote na njia ni salama kwani inapita katikati ya JKT na usalama ni wauhakika

Muhula wa masomo utaanza mwezi …………….., hivyo fika mapema iwezekanavyo ili shule ikifunguliwa tarehe ……………, masomo yataanza mara moja na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe ………………**..**

Shule ya sekondari Muyovozi inatoa masomo katika tahasusi nane ambazo ni **EGM,HGE,KLF,HLF,HGF,HGL,HGK na HKL**.Hivyo una karibishwa katika tahasusi uliyochaguliwa kujiunga nayo.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

a) Sare ya shule kwa; **WAVULANA** ni suruali nyeusi 2 au zaidi na bluu mpauko (light bluu) 2 au zaidi zenye marinda mawili na upana chini uwe wa inchi kumi na saba (17’) na mifuko miwili mbele na mfuko mmoja nyuma (**Modo na zisizo na marinda hazirihusiwi)** mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi, mashati mawili au zaidi meupe yenye mikono mirefu yasiyo na urembo au maandishi yoyote na tai mbili nyeusi na bluu mpauko(light bluu) mbili zinazofanana na kitambaa cha suruali na usinunue spesho. **WASICHANA** ni sketi nyeusi 2 au zaidi na bluu mpauko (light bluu) 2 au zaidi ndefu zinazofikia jicho la mguu zenye rinda boksi mbele na nyuma na sio V ya mbele, mashati meupe 2 au zaidi yenye mikono mirefu yasiyo na maandishi au urembo wowote, tai 2 za bluu mpauko na tai 2 nyeusi. Kwa **wasichana wa kiislamu** sharti nyeupe 2 au Zaidi na juba nyekundu 2 na nyeupe 2 au zaidi zinazo funika kifua zisizo na maandishi au urembo wowote. Na zisifunike tumbo **kamwe vinginevyo hutapokelewa shuleni kabisaa.**

b) Viatu vya kufunga na kamba jozi mbili (2) au zaidi vyenye visigino vifupi

c) Nguo za kushindia:

T-shirt nyeupe yenye rangi ya bluu kwenye kola na mikononi na gauni ndefu zinazofikia jicho la mguu zenye rinda boksi mbele na nyuma rangi damu ya mzee ya kitambaa kizito kwa ajili ya shughuli za nje ya darasa, soksi nyeupe jozi tatu au zaidi zisizo na urembo au maandishi yoyote kwa **wasichana** na nyeusi jozi 3 au zaidi kwa wavulana zisizo na urembo au maandishi yoyote.Pia **wavulana** waje na suruali za nje ya darasa zenye rangi damu ya mzee kitambaa kizito cha kushona na siyo spesho zenye marinda mawili na upana chini uwe wa inchi kumi na saba (17') na mifuko miwili mbele na mfuko mmoja nyuma (**Modo na zisizo na marinda hazirihusiwi)**

d) Sweta rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya baridi liwe zito kulingana na afya yake (hakuna makoti au masweta ya aina nyingine yoyote yatakayo ruhusiwa)
e) Mavazi ya michezo ni bukta/sketi ya bluu zisizo na marinda (solo) ambazo hazina marembo au maandishi yoyote na T.shirt nyekundu zenye kola nyeusi na ufito mweusi mikononi na kwenye mfuko zisizo na maandishi yoyote kwa wote, raba kwa wasichana na viatu vya michezo kwa wavulana.Pia wote (wasichana na wavulana) waje na tshirt(jezi) ya michezo rangi nyeusi na bukta yake.
f) Viatu vya tope (rainboot) na mwavuli
g) Tracksuit ya rangi ya bluu kwa **wasichana** na rangi nyeusi kwa **wavulana** zisizo za kubana au marembo na **zisiwe na kofia ya kuvaa kichwani** zenye ufito mweupe ubavuni

### 2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari kubwa 12 ( counter books( **3 au 4 Quires**)
ii. Kalamu za bluu/nyeusi za kutosha,penseli,rula na mkebe wenye vifaa ;
iii. **Ream (A4)( DOUBLE A au PREMIERS)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mhula;
iv. Vitabu/Vitini vya masomo ya tahasusi husika;
v. Scientific Calculator;(wanaosoma HGE,HGL,HGF,HGK na EGM)
vi. Godoro 2½ kwa 6 aina ya **Dodoma/Banco** tu na siyo malaika;
vii. Mashuka Jozi 2 (rangi bluu bahari),mto wa kulalia na foronya yake rangi ya bluu bahari , blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*bluu) ya pembe nne ikiwa na pini zake za kufungia;*

viii. Nguo za ndani za kutosha,taulo, nguo za kulalia na ndala za kuogea;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Taa au tochi ( inashauriwa anunue taa ya kuchaji kwa jua) kwa tahadhari au dharura
xii. Kwanja1 lililonolewa(**kwa wote**)
xiii. Mfagio wa ndani (**soft broom**) kwa wote
xiv. Rake 1 (**kwa wavulana tu**)
xv. Panga lililonolewa kwa wasichana tu
xvi. Jembe1 lenye mpini na mopa 1 (ya kudekia yenye mti na raba yake) **kwa wote**
xvii. Mfagio (**hardbroom** ) **kwa wote**
xviii. Mfagio (**chelewa**) mmoja wenye mti wa kushikia **kwa wote**.

**2.3.Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Angalizo: Michango hii yote ilipwe kwenye account ya shule hii:MOYOVOZI SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCOUNT NO. 51410006450 NMB na siyo vinginevyo.Uje na benk pay slip iliyoandikwa jina la mwanafunzi**

**NB:**Mwanafunzi awe na Bima ya afya ya NHIF au yoyote iliyoelekezwa na Bima ya afya.Shule inaweza kuwasaidia wanafunzi kupata Bima za vikundi ambavyo vinatambuliwa kwenye hospitali na vituo vya afya vya serikali tu.Hivyo anaweza kuja na fedha taslimu tsh.10,000/= ili kumwezesha kupata kadi hiyo kwani jukumu la afya ya mwanafunzi ni suala la mzazi/mlezi na shule haina mfuko wa kugharamia matibabu kwa mwanafunzi.

**Pia shule haina chakula maalumu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.Hivyo chakula kinachotolewa ni kwa mjibu wa mwongozo uliotolewa na serikali tu.**

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na asubuhi( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kunyoa nyweleziwe fupi na nadhifu tu na siyo vinginevyo
viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
x. Kutunza mali za shule;
xi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwanafunzi/ mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na **nywele fupi** wakati wote wawapo shuleni.**Ni marufuku mwanafunzi wa kiislamu kutumia mwavuli wa kuwa na hijabu kusuka nywele na ukibainika utafukuzwa shule mara moja na kama sharti hili litakuwa gumu kwako omba ubadilishiwe shule mapema**
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya kimapenzi kwa wavulana na wasichana ama jinsi moja


xi. Kuoa au kuolewa;
xii. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xiii. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule;
xiv. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xvi. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule tofauti na zilizoelekezwa na mkuu wa shule;
xvii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;
xix. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xx. Kufanya biashara shuleni ya aina yoyote
xxi. Kujihusisha na ukatili ama unyanyasaji wa kijinsia kwa namna yoyote ile ukiwa shuleni ama nje ya shule

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha(passport size) nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne(school leaving certificate) na Result slip
vi. Cheti cha kuzaliwa(birth certificate) ni cha **lazima na mwanafunzi akija bila cheti hiki hatapokelewa shuleni**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**




**NHIGA J.MWANDU**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0757932910/0622032538**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0612713058**
- **Mwandamizi Taaluma 0627058363/0763429259**
- **Mwandamizi Malezi 0744464130**

# FORM FOR MEDICAL EXAMINATION - FORM A

# MUYOVOZI SECONDARY SCHOOL

# P.O.BOX 463- KASULU

(To be filled by medical officer in respect of all form five entrants)

Student's full name ………………………………………………………..

Age ……………………………………………………………..

Blood count (Red and white) ………………………………..

Urine analysis ……………………………………………

Syphilis test ……………………………………….

T.B test ……………………………………………….

Eye test…………………………………………………….

Ears…………………………………………………….

Chest ………………………………………………..

Spleen ………………………………………………….

Abdomen ……………………………………………..

Additional in formations e.g. physical defects of impairment (s) infection chronic or family diseases.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………….

I certify that the above is fit to nurse as stated above

Signature ………………………………………………..

Date ……………………………Station……………………….

Note : Medical officer : At time of examination please treat the individual for any ailments you note.

N.B : This completed form should be sent to school with your acceptance form or brought when you come to School. No student shall be enrolled without certificate of Physical fitness

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI MUYOVOZI**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI FOMU -B**

1. Jina la mwanafunzi..........................................................Dini / dhehebu ……………………….
2. Jina la Baba …………………………………………..
3. Je! Baba yu hai au alifariki? …………………………………
4. Kama alifariki , taja tarehe au mwaka aliofariki……………………………….
5. Jina kamili la Mama ……………………………….……………….
6. Je! Mama yu hai au Alifariki?...............................................
7. Kama alifariki , taja tarehe au mwaka aliofariki……………………………………………
8. Anuani ya mzazi na namba ya simu inayopatikana mda wote…………………………………….
   Jina la kijiji / mji ………………………………S.L.P ……………………
9. Kazi aifanyayo Baba …………………………………………
10. Sehemu anapofanyia kazi …………………………………..
11. Kazi aifanyayo Mama…………………………………….
12. Kama huishi na mzazi wako , taja jina la mlezi wako
13. Sehemu anapofanyia kazi……………………………………..
14. Kazi aifanyayo mlezi wako …………………………………….
15. Sehemu anapofanyia kazi ……………………………………..
16. Anuani ya mlezi na namba ya simu inayopatikana mda wote………………………………
    Jina la kijiji /mji ………………………………… S.L.P …………………….
17. Habari nyingine za familia,
    Jina la kaka/ dada umri kazi yake mahali anapofanyia kazi kama ni mwanafunzi taja shule
    i) …………………………………… ………………………….. ………………………………..
    ii) ……………………………….. ………………………… ………………………………..
    iii) ……………………………….. ………………………….
18. Afya ya mwanafunzi (tafadhali eleza kuwa una ugonjwa wowote ambao unakukabili kwa hiyo unastahili huduma muhimu). Ni muhimu umfahamishe daktari atakaye kupima ili naye aweze kujaza katika sehemu inayo mhusu kwenye fomu kwa ushauri zaidi wa kitaalamu.
    ..........................................................................................................................................
    ………………………………………………………………………………………………
19. Uthibitisho wa mwanafunzi:-
    Nathibitisha kuwa maelezo niliyo andika katika fomu hii ni sahihi
    Jina kamili la mwanafunzi……………………………………………………………………
    Saini …………………………
    Tarehe ……………......................

**FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE -FOMU C**

Mimi mzazi wa ……………………………………………………………………..

Naahidi kukubaliana na sheria na taratibu zote za shule wakati wote mwanangu atakapokuwa anasoma hapa shuleni.Kwamba mwanangu atafuata na kutii kwa muda wote KANUNI na SHERIA zote zifuatazo za shule hii.

**NI MARUFUKU:-**

1. Kuanzisha / kushiriki kwenye migomo , fujo au ukaidi wa aina yoyote , daima nitatumia taratibu halali ili kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyojitokeza.
2. Kuharibu kwa makusudi mali ya Uma , picha za Viongozi wa serikali na bendera ta Taifa
3. Kuiba
4. Kuwa mwasherati
5. Kutumia kileo na pombe ya aina yoyote
6. Kuvuta sigara au bangi na madawa mengine ya kulevya.
7. Kupatikana na makosa ya jinai
8. Kupata au kutoa mimba na kusababisha mimba ndani na nje ya shule
9. Kupigana , kutoa matusi au matumizi ya lugha mbaya.
10. Kutoroka au kutokuhudhuria shule bila taarifa maalum.
11. Kwenda nje ya shule bila SARE , au Ruksa ya mwalimu yeyote Yule.
12. Kuoa au kuolewa
13. Kuwa mvivu katika kazi za mikono , darasani na wakati wa michezo.
14. Kuchelewa shuleni na kutokufuata Ratiba ya shule kuanzia asubuhi hadi jioni.
15. Kwa mwanafunzi kwa kutojiheshimu mwenyewe na kutoheshimu watu wengine . Salamu kwa kila anayekuzidi umri ni muhimu na kutokufanya hivo utachukuliwa kama utovu wa nidhamu .
16. Kutokurinda na kutunza siha yako ya usafi na mazingira ya shule.
17. Kutokufanya mitihani yoyote ya ndani na nje
18. Kwa mwanafunzi kutokulinda , kutunza au kuharibu mali ya shule . Uharibifu na upotevu wa mali yoyote itakubidi ulipe gharama za uharibifu au upotevu huo
19. Mvulana na msichana kuishi chumba kimoja
20. Kukataa adhabu kwa makusudi
21. Kumiliki au kuwa na simu ya mkononi
22. Kwenda kwenye miji ya walimu bila wito wa mwalimu husika .
23. Uzurulaji wa mitaani kumbi za starehe , mabanda ya video , baa , vijiwe vya michezo ya mitaani kama vile , pool table , bao , karata ,drafti n.k.

Endapo mwanangu atavunja sheria mojawapo kati ya hizo nitakuwa tayari kushirikiana na uongozi wa shule na kusimamia adhabu atakzopewa mwanangu kati ya zifuatazo:-

Kuchapwa viboko(visivyozidi vinne kwa kulingana na kosa)

i) Matakoni (wavulana ) kwa kulala chini

ii) Mikononi (wasichana) kwa kunyosha mkono bila kukwepesha

a) Kufanya kazi ngumu kama vile , kutengeneza barabara , kuchimba shimo la takataka , kufyeka nyasi/ vichaka , kuokota mawe n.k.
b) Kupewa onyo kali kimaandishi
c) Kusimamishwa shule kwa muda usiozidi siku 21.
d) Kufukuzwa shule na bodi ya shule.

**MWISHO:** Gharama zote za kwenda nyumbani na kurudi shuleni ni jukumu langu na nitalitimiza kwa wakati ikiwa ni pamoja na kulipia michango iliyokubalika

Saini ya mzazi/ mlezi ……………………………. Tarehe …………………………..